



22130197



SWAHILI A: LITERATURE – HIGHER LEVEL – PAPER 1
SWAHILI A : LITTÉRATURE – NIVEAU SUPÉRIEUR – ÉPREUVE 1
SWAHILI A: LITERATURA – NIVEL SUPERIOR – PRUEBA 1

Wednesday 8 May 2013 (morning)
Mercredi 8 mai 2013 (matin)
Miércoles 8 de mayo de 2013 (mañana)

2 hours / 2 heures / 2 horas

INSTRUCTIONS TO CANDIDATES

- Do not open this examination paper until instructed to do so.
- Write a literary commentary on one passage only.
- The maximum mark for this examination paper is *[20 marks]*.

INSTRUCTIONS DESTINÉES AUX CANDIDATS

- N'ouvrez pas cette épreuve avant d'y être autorisé(e).
- Rédigez un commentaire littéraire sur un seul des passages.
- Le nombre maximum de points pour cette épreuve d'examen est *[20 points]*.

INSTRUCCIONES PARA LOS ALUMNOS

- No abra esta prueba hasta que se lo autoricen.
- Escriba un comentario literario sobre un solo pasaje.
- La puntuación máxima para esta prueba de examen es *[20 puntos]*.

Andika uchambuzi kuhusu kifungu **kimoja** kati ya hizi:

1.

- “Usibabaike mwenzangu. Usitake kukipeleka kilio matangani ukalia hata kuliko wafiwa. Waama mja akishautafuna utamu wa muwa ganda atalitakia nini? Lisilo budi hubidi, au siyo? Hali kadhalika wewe ni mjumbe na tangu lini mjumbe akauwawa? Tumechuana na kazi kwa ajili ya wanafunzi mwaka wote na panapo majaliwa matokeo yao yatakuwa sheshe bila shaka.
- 5 Hata hivyo ieleweke kwamba dunia ni mduara huzunguka kama pia. Hatuwezi kuwa mahali pawili kwa wakati mmoja. Kwamba tulikuwa hapa Kilelecha-Karen, basi tusingekuwa kwingine. Hicho ni kitendawili kwenu kama viongozi wa afisi zenu hapa. Sina kinyongo wala fundo moyoni lakini mbona mkurugenzi Skolastika Majungu atukumbushaye kuwa waadilifu, leo hii anaukokotea uadilifu uo huo matopeni kisha kutupokezea katika mavazi yetu ya sherehe?
- 10 Mbona akawa akina penyenyeza shule kuuzwa kama mlanguzi wa afyuni aliyefumaniwa na walinda usalama? Sisononeki. La hashu! Ushikwapo shikamana ukiangukwa lalama. Hatuwezi kudai kuwa jeta eti hatubanduku papa hapa Kilelecha-Karen. Ni dhahiri shahiri kuwa hapa Kilelecha si mbinguni na kule nje siko jehnamu. Mungu haishi hapa tu wala makao ya shetani siko kule nje. Jambo muhimu ni kuwa, hesabu siku zilizobaki kufikia sherehe
- 15 za krismasi. Wakati huu nafasi zote za kazi katika shule zozote zile hapa mwakani zimezibwa kwa vizibo kama vya chupa za champeni. Hakuna mpenyo. Nana Skolastika Majungu ndiye mkurugenzi asifiwaye kuwa ndiye mfano tosha wa ustaarabu na maendeleo? Kila apitapo akiinamiwa na kuitwa Mama! mama! Ni mama yupi ang’wafuaye minofu na kuwaachia wanawe kuguguna mifupa mitupu? Labda yake yawe ni maendeleo ya...”
- 20 Chapakazi hakumaliza sentensi hiyo. Alijiona ni kama msafiri ambaye amekamilisha awamu nyingine tu ya safari yake katika pululu zenye wingi wa nunda wala watu. Lahaula! Sasa ukiingia kwenye pori lenye majuju wa majuju wenye raghba ya kutafuna mifupa ya binadamu na kufyonza uboho...! Kwa mara nyingine tena aliotoswa katika bahari ya papa, papaupanga na milima ya mawimbi. Afua ilikuwa mbili, aogele dhidi ya yale mawimbi afike
- 25 salama ng’ambo ya pili la sivyo ang’atwe na kung’wenywa na papa afe akipiga siahi huku akiiona damu yake mwenyewe ikiipa bahari ya samawati rangi ya wekunduwekundu. Alihisi uchungu mkubwa. Kweli johari za mtu ni mbili, akili na haya. Akili ilimkumbusha kuwa asipyole kwa kuwa mchama ago hanyeli huenda akuaya hapo. Haya nayo yalimkataza kujipembejea japo uchungu ule ukimpekecha mifupani na kumsugua moyoni.
- 30 Hata hivyo, alihisi nafuu ya kufuja kwa pakacha la mchukuzi kwa kuondoka Kilelecha-Karen lakini taharuki na wasiwasi wa mwasi mbioni kwa alikotarajia kwenda. Eti sasa alikuwa miongoni mwa wasiokuwa na ajira? Hivyo tu! Alicheka. Alicheka kweli? Huenda alikenua tu na kupiga kite. Taswira ya wanawe na mke wake kipenzi ilimpita kichwani. Je wakati huo huo walikuwa wapi na walikuwa wakiwaza nini...? Kweli maisha yao yalikuwa ni fumbo.
- 35 Wengine wakiimba waziwazi namna aila zao zilivyoogelea katika uhondo wa maisha, mwalimu Chapakazi lake lilikuwa kuwatumbulia jicho tu. Si ajabu basi habari za jamaa yake hazikujulikana sana-siri yake.

Aliyoyaona hapo Kilelecha-Karen, yaliuviza moyo wake wa imani kwa mabwanyenye waliodai ni wakurugenzi. Ukurugenzi wa ukatili, unyanyasaji, uumbuaji, udhalilishaji na udharishaji wa walimu. Aliwafananisha na tai wanaodona na kung’wafua mizoga ya utashi wa walimu; kisha wakageuka fisi kuiguguna na kuusaga utule wa wahasiriwa wakipasua vicheko huku wakijisombogoa kwa miondoko ya densi ya Salsa. Mwisho wakaufyonza uboho wa mifupa na kwa kuwatupilia mbali katika hewa yabisi. Kwao si hoja. Si ni kweli kuwa kuna majalada yaliyojaa maombi ya waalimu wenye hamu ya kufunza mfano wa kumbikumbi wapao kuuendea mwangaza.

Kwao wakurugenzi, mwalimu hana hadhi bali ni kama ombaomba aliyejisiriba kewa kinyaa. Kuwepo kwake kazini ni kutaka tu kumtapisha mhisani wake-mkurugenzi. Kwa hiyo nafuu ya mhisani ni kumuokotea ombaomba huyo makombo na masazo mengine na kumtupia angaa amuondokee upesi. Mshipa haukumpiga mkurugenzi kuwa mwalimu hakuwa ombaomba wa kawaida kwani kutwa nzima alikuwa amejipinda mgongo kondeni kuiimarisha mimea iliyokuwa imesongwa na magugu. Mimea ambayo ingemhakikishia mkurugenzi msimu wa kazole. Potelea mbali alimvurumisha mwalimu makondo hayo. Ndio, mwalimu ayachukue au ayawache katika unyonge wake ule wa, “nisimbulie unipe, mtashi hana kinyongo”.

Anduvate K Mwavali, *Kifo cha mwalimu* (2011)

2.

Wakati titi la nyati

Wakati johari njema, hasa ule wa bahati,
Wakati wenye neema, mtu huwa ithibati,
Wakati uwe salama, raha hupanda makuti,
Wakati titi la nyati, hukamuliwa kwa shaka.

5 Wakati mwana rehema, mvulana na benati,
Wakati wenye huruma, mtamu kama wa titi,
Wakati njoo mapema, usiku kuna vijiti,
Wakati titi la nyati, hukamuliwa kwa shaka.

10 Wakati ni wa karima, ndiye mtoa sharti,
Wakati Mungu apima, yeye Raufu Ladhati,
Wakati ni wa kusema, na kauli ya kaputi,
Wakati titi la nyati, hukamuliwa kwa shaka.

15 Wakati ni wa kuchuma, Jaala Wabarakati,
Wakati hufanywa bima, sipukutike pukuti,
Wakati hutia homa, ukikutegua futi,
Wakati titi la nyati, hukamuliwa kwa shaka.

20 Wakati mwana yatima, pato lake ati ati,
Wakati huwa ni chuma, huzikata mifumbati,
Wakati huja adhima, mnyonge kupewa kiti,
Wakati titi la nyati, hukamuliwa kwa shaka.

Wakati unasimama, huenda paka Babati,
Wakati na huinama, ukaenda kwa magoti,
Wakati huja kuhama, ukabakia katiti,
Wakati titi la nyati, hukamuliwa kwa shaka.

25 Wakati bahati nyuma, yakuacha katikati,
Wakati una dhuluma, kukutenga kizingiti,
Wakati hauna pima, huja kutatiza tati,
Wakati titi la nyati, hukamuliwa kwa shaka.

30 Wakati huwa tuhuma, kunyonya ziwa la nyati,
Wakati huwa zahama, upitapo na hupiti,
Wakati mwisho nakama, ukayatema matiti,
Wakati titi la nyati, hukamuliwa kwa shaka.

Wakati kama mnyama, vyepesi kukusaliti,
Wakati hauna mwema, huja nyuma kama koti,
35 Wakati tena hukoma, uanguke kama mti,
Wakati titi la nyati, hukamuliwa kwa shaka.

Wakati ni kaditama, ogopa vita kuzatiti,
Wakati huja kuzama, ukuache umeketi,
Wakati ni kuchegana, ni mwisho wa zangu beti,
40 Wakati titi la nyati, hukamuliwa kwa shaka.

Mathias Mnyampala, *Diwani ya Mnyampala* (1965)
